JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAISI - TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI NYAKAHURA
S.L.P 195
TAREHE 12/05/2018

Namba za simu
Mkuu wa shule . 0766235699
Makamu mkuu wa shule . 0787201405

Mzazi/ Mlezi wa mwanafunzi…….
……..
…….
S.L.P……
……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYAKAHURA ILIYOPO HALMASHAURI YA BIHARAMULO MKOA KAGERA MWAKA 2018

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2018 shule ya Sekondari Mubaba ipo umbali wa kilometa 75. Mashariki mwa mji wa Biharamulo.

Muhula wa masomo unaanza tarehe 18/07/2018. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shule tarehe 18/07/2018 mwisho wa kuripoti ni tarehe 01/8/2018 .

Mambo muhimu ya kuzingatia :-

Sare ya shule

Sare ya shule hii ni mashati meupe 2 mikono mifupi na sketi 2 rangi nyeusi kwa wasichana zenye linda nane na belt inchi tatu na mashati meupe 2 mikono mifupi na suruali 2 rangi nyeusi zenye linda mbili kila upande ziwe za kuvaliwa kiunoni nap indo la chini (Turn –up) mkanda mweusi wa ngozi kwa wavulana usiokuwa na urembo wowote.

Rangi ya hijabu (kijuba) ifanane na sare ya shule

Sare ya michezo kwa shule hiini T- shirt /jezi za rangi ya blue , bukta ,Track suit, raba na soksi / stockings za michezo.

Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.

Soski jozi mbili nyeupe

Sweta ya shule inapatikana shuleni

T- shirt ya shule inapatikana shuleni

Nguo za kushindia (shamba dress) gauni 2 rangi ya pink zinapatikana shuleni kwa (wasichana) na suruali ya rangi ya damu yam zee yenye sifa kama sare ya shule (wavulana)

Ada na michango ya shule

Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000.00 kwa wanafunzi

Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000.00 kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. (Tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye PAY IN SLIP)

(b)Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni;

i. Shilingi 15000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha
iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma
iv. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi , walinzi na vibarua wengine.
v. Shilingi 2,000/= kwa nembo ya shule
vi. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza
vii. Tshs. 5,000/= Bima ya Afya
viii. Shilingi 20,000/= Mitihani ya kujipima mock
ix. Fedha ya tahadhari 5,000/= (haitarejeshwa)

(c) mahitaji muhimu ambayo manafunzi anapaswa kuleta shuleni ni :-

i. Ream ya karatasi 1 (kwa mwaka)
ii. Vitabu vya masomo ya tahasisi (combination) husika ya mwanafunzi.
iii. Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia
iv. Scientific calculator
v. Godoro kwa wanafunzi wa bweni futi 3
vi. Mashuka pair 2 ya rangi ya light blue, blanketi 1, foronya 1, chandarua 1.
vii. Vyombo vya chakula (sahani , bakuli , kijiko na kikombe)
viii. Ndoo mbili kubwa zenye mifuniko
ix. Kwanja 1, jembe 1 na mpini , reki 1, mifagio ya ndani na nje
x. Dawa ya chooni lita 5
xi. Aje pia na mahitaji mengine muhimu kwa wasichana .
xii. Mwanafunzi anatakiwa aje na picha 4 za wazazi, ndugu wa karibu wanaoweza kutembelea shuleni hapa.

(d) Kulingana na mazingira ya shule yangu bodi ya shule imekubaliana mwanafunzi anatakiwa kuchangia fedha katika maeneo yafuatayo:-

1. Shilingi 25,000/= kwa ajili ya kiti na meza
2. Shilingi 25,000/= kwa ajili ya kitanda
3. Shilingi 50,000/= kwa ajili ya ujenzi wa miundo mbinu

4. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi , kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika . Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozo wa shule .
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
viii. Uvutaji wa sigara
ix. Uasherati , uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu , siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
xiii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xiv. Kumiliki ,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xv. Kudharau Bendera ya Taifa
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiunga , au kutishia kujiua kama kunywa sumu.
xvii. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

5. viambatanishi na fomu muhimu
    a) fomu ya Uchunguzi wa Afya (medica Examination Fomu) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.

N.B

Ili kuepusha usumbufu vitu vifuatavyo vinapatikana shuleni kwa bei nafuu.

i. Godoro futi 3
ii. Ream ya karatasi
iii. Ndoo mbili kubwa zenye mifuniko
iv. Kwanja 1, jembe 1na mpini , reki 1, mifagio ya ndani na nje.
v. Scientific calculator
vi. Graph pad, Beseni
vii. Nguo za michezo truck suit light blue

R.ISHENGOMA
MKUU WA SHULE

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SHULE YA SEKONDARI ……
S.L.P……
BIHARAMULO
12/07/2018

FOMU

MGANGA MKUU WA KOA , WILAYA , KITUO CHA AFYA

Jina ……. Amechaguliwa kujiunga na kidato cha ……. Katika shule hii , ili kuendelea na masomo ni lazima apimwe kwanza.

Nitafurahi iwapo mbali na kupimwa kijana huyu ataangaliwa uwezo wa kuona macho yake. Kama imeshauriwa avae miwani hana budi kuinunua yeye mwenyewe kwa fedha yake .

Tafadhali nijazie sehemu inayohusika chini baada ya kupima .

Asante kwa ushirikiano

……..
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI……..
S.L.P……..
BIHARAMULO

Nimepima mwanafunzi aliyetajwa hapo juu nakuona kwamba ana matatizo / ugonjwa wa:-

A. Kifua kikuu……
B. Macho……
C. Masikio……..
D. Akili…….
E. Kilema chochote……..
F. Choo……..
G. Kwa wasichana tu nimeona / hana mimba……
H. Mengineyo …….

SAINI MHURI WA OFISI ……

MGANGA MKUU WA MKOA / WILAYA / KITUO CHA AFYA……

FOMU YA KUANDIKISHWA – SHULE

(Ijazwe kwa herufi kubwa na irejeshwe kwa mkuu wa shule)

1. Jina kamili ……..
   Tarehe ya kuzaliwa …… Wilaya ……Mkoa ……..
   Taifa …….Dini:Rc/Anglican /Lutheran/Muslim/Petecoste n.k
   Shule ya sekondari unayotaka ……..
2. Jina la Baba / Mama /Mlezi …….
   Anwani yake……..
   Kazi ya Baba / Mama /Mlezi ……..
   Namba ya simu……
3. **AHADI YA MWANAFUNZI**
   - **a.** Mimi ……..nimeyasoma na kuyaelewa maelekezo yote ambayo ni pamoja na sheria na kanuni za shule na nimekubali kuingia kidato cha tano katika shule ya sekondari …….. kuanzia tarehe……hadi nitakapo maliza kidato cha sita.
   - **b.** Kwa hiyo naahidi kwamba:-
     i. Nitazitii sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa
     ii. Sitashiriki vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi wa serikali ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania
     iii. Nitatunza mali ya umma ambayo ni pamoja na majengo, samani , vitabu n.k

Tarehe …… saini ya mwanafunzi……..

4. AHADI YA MZAZI / MLEZI
   Mimi…….amabye ni mzazi / mlezi wa mwanafunzi …….ninahaidi kwamba:-
   i. Nitashirikiana na Uongozi wa shule , walimu na watumishi wasio walimu katika kuhakikisha , mwanangu anatii sheria na kanuni za shule ya sekondari …… Na iwapo atashindwa kutii sheria hizo, nitalazimka kumuondoa katika hosteli.
   ii. Nitafanya kila niwezalo kumwezesha mwanangu, kusoma kwa kulipa Ada na michango mingine kama ilivyoelekezwa na shule.

Tarehe …… Saini…….namba ya simu :……

N.B

Uongozi wa shule unakutakia maandalizi mema na safari njema ya kuja hapa shuleni

NACHUKUA NAFASI HII TENA KUKUPONGEZA NA KUKUKARIBISHA

Wako katika Ujenzi wa Taifa

R.ISHENGOMA

MKUU WA SHULE